# PIGENI KELELE ZA FURAHA

Yes 12,2-3,4,5-6 siku ya Mungu ya tatu ya majilio

Musique: Alphonse LEBON




R/ Pigeni kelele za furaha na shangwe , maana ametukuzwa ndani yetu Mtakatifu wa Israeli x2

1. Sasa Mungu ni mwokozi wangu
   namtumainiya, wala sinahofu tena
   kwa kuwa ni nguvu yangu na wimbo wangu
   Bwana amekuwa wokovu wangu

2. Nanyi mtachota maji kwa furaha, visimani mwa wokovu
   Mtukuzeni bwana, liombeni jina lake
   tangazeni matendo yake kati ya mataifa
   wakumbusheni yakuwa jina lake ni tukufu

3. Mwimbiyeni Bwana, maana ametenda makuu
   nayo yatangazwe duniani kote
   pigeni kelele za furaha na shangwe, wenyeji wa sioni
   maana ametukuzwa ndani yenu Mtakatifu wa Israeli